# HEKALUNI TWENDE

B N Mogeni
09/02/2023






2. Ndege wa angani walia kwa sauti zao tamu,
   kuashiria kumekucha twendeni tumuabudu,
   mashariki tukitazama jua nalo lachomoza,
   kuonyesha ni siku mpya twendeni tumuabudu.

3. Ametulinda siku wiki miezi sasa miaka,
   tuingie nyumbani mwake twendeni tumuabudu,
   ametuvusha na vikwazo vyake muovu shetani,
   tumefika siku ya leo twendeni tumuabudu.

4. Vipaji mbalimbali Mungu akatujalia sisi,
   yatupasa tumshukuru twendeni tumuabudu,
   njoni wapendwa tumuombe neema nazo baraka ,
   atuzidishie ili tumtumikie milele.


2